

Mabadiliko katika fasihi simulizi ya wagogo

May L.Y. Balisidya

(Bibi MATTERU)

Tasnifu ya digrii juu katika sayansi jamii

Chuo kikuu cha Dar es Salaam, Institute of Kiswahili studies 1977.

Tasnifu hii ina lengo la kuonyesha kuwa. ingawaje fasihi simulizi hutumiwa na jamii kisanaa kujieleza na hivyo kuielekeza na kuiendesha, hujengwa, na ni zao la jamii hiyo na mabadiliko yake. kwa hivi hutokea kuwa Itabadilika pamoja na jamii na katika kubadilika huku, itadhihirisha yale mabadiliko yanayoifika jamii, Fasihi simulizi haiachani na mwenendo wa jamii katika nyakati na maendeleo yake. ina ukongwe katika upokezi wa sanaa yenyewe, kama sanaa nyingine, hii sanaa iendayo wakati. Pia ni lengo la tasnifu hii kuuzingatia umiliki wa jamii wa fasihi simulizi na nafasi ya fanani wa fasihi hiyo katika jamii. Fasihi simulizi ni mali ya jamii kidhamira na kiutoaji, na kila mtu ana fursa ya kumiliki na kuzitumia tanzu mbali mbali. Fasihi hii ina fanani wake ambao hupewa hadhi kutegemea na nafasi inayopewa fasihi wanayo jihusishanayo

1/ Tafasi ipewayo fasihi hiyo hutegemea dhima yake katika jamii yenyewe na jinsi gani fanani anaiwezesha fasihi hiyo kuitekeleza dhima hiyo. kwa hivi fasihi na fanani wake wataangaliwa katika nafasi na dhima yao katika nyakati mbali mbali za mabadiliko ya jamii.

Kwa vile hivi sasa fani nyingi za fasihi hii zimo katika Lugha za makabila, ili kuyakinisha kazi ya tasnifu hii, jamii ya Wagogo imeteuliwa kufanylwa uchunguzi. lakini, hata huko Ugogoni, fani za fasihi Birnuzi zimetamba katika: nathari, ushairi na semi kiasi kwamba kuziingiza zote katika tasnifu hii kutakuwa ni kurudufu mambo yanayozungumziwa kwa hivi, tanzu moja tu imeteuliwa kuehunguzwa ili inasibishe hoja zilizotolewa hapo juu. Tanzu hii ni hadithi.

”Hadithi” kwa mujibu wa tasnifu hii ni tanzu nzima ya fasihi simulizi ambayo inazo fani mbali mbali ndani yake. Hadithi, itakuwa ni aina ya fasihi inayojihusisha na usimulizi katika umbo la nathari (lugha ya ujazo ya maongezi ya kila siku). Usimulizi ambao hupangwa katika mtiririko wa vituko unaokamilisha kisa/visa 2 fulani. igawanyo huu umetokana na mijadala ya Mwaka wa III, Idara ya Kiswahili Chuo Kikuu cha Dar es Salaam 1975/76. Ruth Finnegan katika oral Literature in Africa, The Clarendon Press. oxford, 1970 anagawanya Fasihi Simulizi katika sehemu tatu: Ushairi, Nathari na Fani Nyinginezo. Fani ya Semi kwa mujibu wa tasnifu hii ni tungo fupi fupi zenye uzito wa taswira, aghalebu zenye mafunzo na maadili mathalan: methali, misemo, nahau, misimu vitendawili n.k.

Kisa ina maana ya mfululizo wa vituko unaokamilisha maelezo juu ya tukio fulani,

Wahusika ndio nyenzo zitumiwazo (kwa kutenda, kutendewa na kujengwa kusimamia hali maridhawa za binadamu). Wao huzungumza, huzungumziwa na huzungumzishwa katika lengo la kutoa dhamira, maadili, ujumbe na falsafa zitakiwazo na mtunzi wa hadithi. kwa dhana hii, hadithi Ugogoni ina maumbo matatu: Simo Nghomo na Mbazi.

Hata katika uteuzi wa tanzu hii, kulitafiti şuala la fasihi simulizi kama hilibyooneshwa, fani mbili tu zimeteuliwa kushughulikiwa, nazo ni Simo na Nghono. Hizi zinechaguliwa kwa vile ndizo kuu katika tanzu hii. Mbazi hazitashughulikiwa na tasnifu hii kwani si maarufu sana za huondokea kutungwa papo kwa papo zaidi kutegemea ufundi wa binafsi katika mazingira yanayo husika. mifano itakayotuniwa katika tasnifu hii itatolewa katika tafsiri sisisi ili isipoteze ladha, usanii na maana yale katika Kigogo. tafsiri sabilia itakapotumiwa, ni pale tu ambapo kwa ajili ya kuapata maudhui kiujumla, pamelazimika kutolewa. ufupisho wa mfano mzima. Tasnifu yenyewe itagawanyika katika sehemu zifuatazo:

Utangulizi: ambayo jamii ya Wagogo itaangaliwa katika muundo, mahusiano yake, historia na mazingira yake.

Sehemu I

Dhana ya hadithi kama Inavyoeleweka kwa Wagogo itazingatiwa na kugawanywa katika sura mbili kufuatana na fani zenyewe za hadithi.

Sura ya Kwanza: Simo Sura ya Pill: Nghomo

Sehemu II

Kiini cha tasnifu hii kitakuwa hapa. Mabadiliko katika hadithi yataangaliwa kwa kugawanya sehemu hii katika sura tatu.

Sura ya Kwanza: Mabadiliko katika Dhamana na Dhima ya hadithi.